



MWONGOZO WA UHUISHAJI WA HATI YA USAJILI WA JENGO LA FAMASI

1. UTANGULIZI

Baraza la Famasi ni taasisi ya Serikali chini ya Wizara ya Afya iliyoungwa kwa Sheria ya Famasi, Sura 311 na kupewa jukumu la kusimamia taaluma ya famasi na utendaji wa wanataaluma nchini.

Katika kutekeleza majukumu yake, Baraza linasajili Majengo ya kutolea hudumu ya dawa (Famasi) kwa mujibu wa Kanuni za Usajili wa Majengo GN No. 269 ya mwaka 2020; Kwa mujibu wa Kanuni ya 9 inaelekeza kuwa Hati ya Usajili wa JenGO itahuishwa kila baada ya miaka mitano (05) tangu kutolewa kwake. Lengo la kuhuisha usajili ni kuhakikisha kuwa viwango vya ubora wa jengo katika utoaji wa huduma ya dawa unazingatiwa wakati wote.

2. MALENGO

Kutoa ufafanuzi kwa majengo yanayotakiwa kuhuisha hati ya usajili wa jengo.

3. WALENGWA

Majengo yote ya famasi yaliyofikisha miaka mitano (05) tangu yasajiliwe.

4. UTARATIBU WA KUHUISHA

4.1 UKAGUZI WA JENGO

Mfamasia Msimamizi/ Mmiliki wa Famasi:

4.1.1 Kujaza **Fomu PCF 5A** inayopatikana katika tovuti ya Baraza la Famasi na kuiwasilisha ofisi za kanda.

4.1.2 Kulipia ada ya ukaguzi (Inspection fee) kupitia ankara ya malipo itakayotolewa na ofisi za baraza.

Wakaguzi wa kanda, Mkoa na Halmashauri:

4.1.3 Kufanya ukaguzi wa Famasi ili kuhakiki udumishwaji wa vigezo vya jengo husika (Premises standards) kwa kutumia **Fomu PCF.6**.

4.1.4 Ofisi ya Baraza kutoa matokeo ya ukaguzi ikiwa ni pamoja na maboresho yanayotakiwa kufanyika kama yapo.

4.2 UHUISHAJI WA HATI YA USAJILI

Mfamasia Msimamizi/ Mmiliki wa Famasi:

4.2.1 Kujaza fomu ya maombi ya usajili wa jengo (**PCF.12**).

4.2.2 Mfamasia kuhuisha taarifa katika mfumo wa kieletronic (PCMIS) na kuambatisha nyaraka zote zinazohitajika ikiwemo fomu ya maombi.

4.2.3 Kulipia ada ya kuhuisha kupitia ankara iliyotengenezwa katika mfumo.

Ofisi za Kanda za Baraza:

4.2.4 Kuhakiki taarifa zilizowasilishwa katika mfumo.

4.2.5 Kuidhinisha au kutoa mrejesho kulingana na uhakiki uliofanyika

4.2.6 Kutoa hati mpya za usajili wa majengo kwa famasi zilizohuisha

Imetolewa na:

**Ofisi ya Msajili
Baraza la Famasi
2023**